

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)



Simu Na: 026 - 2968433
Nukushi Namba: 026 – 2968832
Tovuti: www.njombetc.go.tz
Barua pepe : td@njombetc.go.tz

S.L.P. 577
NJOMBE.

24/05/2022

Unapojibu tafadhali taja:

KUMB.NA.NTC/E:P/152/522/1B/40

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe anapenda kuwatangazia wananchi wote raia wa Tanzania wenye sifa, kuomba nafasi za kazi zifuatazo:-

DEREVA (Nafasi (3)

Sifa za Mwombaji.

1. Awe Mhitimu na mwenye cheti cha kidato cha Nne (Form IV) na Leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji wa magari ambaye amefanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
2. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya Uendeshaji magari yanayotolewa na chuo cha ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.

KAZI NA MAJUKUMU

1. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
2. Kuwapeleka watumishi katika maeneo mbalimbali ya kazi.
3. Kufanya matengenezo madogo ya gari.
4. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
5. Kufanya kazi nyingine kadri utakavyo elekezwa na msimamizi wako.

MSHAHARA

Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani Mshahara wa TGS B

MHUDUMU WA JIKONI/MESS ATTENDANCE (Nafasi 03)

Sifa za Mwombaji

1. Awe Mhitimu na Mwenye cheti cha kidato cha Nne mwenye uzoefu wa kazi kwa muda usiopungua miaka mitatu (03)

KAZI NA MAJUKUMU

1. Kusafisha vyombo vya Kupikia.
2. Kusafisha vyombo vya kulia chakula.
3. Kusafisha meza itumiwayo kwa kulia Chakula.
4. Kuwatayarishia Wapishi/Waandazi wa vifaa vya Mpishi na Mezani.
5. Kusafisha maeneo ya kulia chakula na kupikia.
6. Kuwasaidia waandazi na wapishi.

MSHAHARA


Kwa kuzingatia viwango vya Serikali yaani Mshahara wa **TGOS A**

MASHARTI YA MWOMBAJI

1. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 40.
2. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.
3. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) Yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
4. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Taaluma, cheti cha kidato cha nne na cheti cha kuhitimu mafunzo ya Udereva.
5. Waombaji waambatishe Picha moja ya Passport size ya hivi karibuni.

Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 06/06/2022 Siku ya Jumatatu saa 9:30 Alasili.

Maombi yote yatumwe kwa;
Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji
S.L.P 577,
NJOMBE.
Imetolewa na;


K.A Sadick
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
NJOMBE.

